

Hati ya Maandishi

Msingi Kutumia data ya uchunguzi kutoka nchi mahususi kuelezea matukio ya janga la maambukizi ya homa ya mafua kunaweza kupelekea uamuzi kuhusu makadirio ya muda wa kutoa chanjo ya homa ya mafua. Tulichambua data ya uchunguzi kutoka nchi za Afrika ili kubaini muda halisi wa janga la maambukizi ya homa ya mafua ya kimsimu ili kufanya mikakati ya kitaifa ya kutoa chanjo.

Mbinu Tulitumia data muhimu ya umma inayopatikana kutoka nchi zinazotoa ripoti kwenye Mtandao wa Uchunguzi na Mwitikio Kuhusu Homa ya Mafua Ulimwenguni (Global Influenza Surveillance and Response, GISRS) kwa data ya miaka 3–10 iliyokusanywa 2010–2019. Tulihasabu mwendo wa wiki 3 wa hali ya maambukizi kutoka kwa kiwango fulani cha sampuli zilizo na virusi vya homa ya mafua na kutathmini muda wa janga la maambukizi kwa kutumia njia ya uwastani wa alama za kiviwango. Mwanzo na mwisho wa kila janga la maambukizi ulifafanuliwa kama wiki ya kwanza wakati kiwango kilizidi au kilipopungua kuliko kiwango cha kadri cha kila mwaka husika, kwa wiki ≥ 3 mfululizo. Tulipanga mataifa kulingana na aina tano za mfumo ya janga la maambukizi: Majanga ya Maambukizi ya Mawio ya Kaskazini (Northern Hemisphere, NH) yaliyotokea kwenye miezi ya Oktoba–Machi, majanga ya maambukizi ya Mawio ya Kusini (Southern Hemisphere, SH) yaliyotokea kwenye miezi ya Aprili–Septemba, kimsingi mawio ya Kaskazini yalikuwa na baadhi ya shughuli za majanga ya maambukizi hayo kwenye miezi ya mawio ya kusini, kimsingi mawio ya kusini yalikuwa na baadhi ya shughuli za majanga ya maambukizi hayo kwenye miezi ya mawio ya kaskazini, na vilevile kulikuwa na maambukizi ya mafua mwaka mzima bila ya utambuzi wowote uliojitokeza waziwazi kwenye mawio ya kaskazini au mawio ya kusini (hakuna mfumo wazi).

Matokeo Kati ya nchi 34 zinazoripoti data kwa FluNet, nchi 25 zimekuwa na angalaa miaka 3 ya data, ikiwakilisha 46% ya nchi za Afrika na 89% ya idadi ya watu wa Afrika. Nchi ambazo utafiti huu ulifanywa ziliripoti matokeo ya virusi vya mfumo wa kupumua RT-PCR kutoka kwa jumla ya sampuli 503,609 (wastani wa 12971 [IQR 9607 – 20960] kwa kila nchi kwa mwaka) ambapo 74001 (15%; wastani wa 2078 [IQR 1087 – 3008] kwa kila nchi kwa mwaka) walipatikana kuwa na virusi vya homa ya mafua. Majanga ya maambukizi 248 yalitokea kwa miaka 236 ya data ya nchi (wastani 10; [uwiano wa: 7–10] kwa kila nchi). Nchi sita (24%) zilikuwa na mfumo wa mawio ya kaskazini (Aljeria, Burkina Faso, Misri, Niger, Morocco, na Tunisia). Nchi nane (32%) kimsingi zilikuwa na mfumo wa mawio ya kaskazini na baadhi ya majanga ya maambukizi kutoka mawio ya kusini (Cameroon, Uhabeshi, Mali, Msubiji, Nigeria, Senegal, Tanzania, na Togo). Nchi tatu (12%) kimsingi zilikuwa na mfumo wa mawio ya kusini na baadhi ya majanga ya maambukizi kutoka mawio ya kaskazini (Ghana, Kenya, na Uganda). Nchi tatu (12%) zilikuwa na mfumo wa majanga ya maambukizi ya mawio ya kusini (Jamhuri ya Afrika ya Kati, Afrika Kusini, na Zambia). Nchi tano (20%) hazikuwa na mfumo wowote wazi (Cote D’Ivoire, DR Congo, Madagascar, Mauritius, na Rwanda).

Ufasiri Nchi nyingi zaidi zilikuwa na vipindi vinavyotambulika vya janga la maambukizi ya homa ya mafua ambavyo vingetumika kufahamisha mamlaka kuhusu shughuli zisizo za kimsimu na za kimsimu za homa ya mafua, kutoa mwongozo wa muda wa mzuri chanjo, na kuhimiza mwingilio kati kwa muda unaofaha.

**Kwa Ajili ya Tafsiri
Lancet Global Health**

Ufadhili Hakuna